

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BAGAMOYO**



**TANGAZO LA ZABUNI YAUOMBAJI WA NAFASI KWA WAFANYABIASHARA**  
**MBALIMBALI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO KWENYE SOKO**  
**JIPYA LA MAGOMENI(MIVARF) KWA MWAKA 2016-2017 na 2017-2018.**

1. Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo inawatangazia wafanya Biasharawenye uwezo wa kutoa Huduma za kufanyabiashara katika soko letu jipya la MAGOMENI kwa mudaunaoanzia tarehe **01/04/2017** hadi tarehe **30 /6/2017 na 01/07/2017 hadi 30/06/2018 kama ilivyoainishwa hapa chini;-**
2. Nafasi zinazotangazwa kwa kipindi hicho ni kama zifuatazo;-  
**ZABUNI ZA MWAKA MMOJA(1)**

NAMBA YA ZABUNI	JINA LA ZABUNI
LGA/014/2016/2017/NC/01	Ukodishaji wa vizimba, nafasi 70
LGA/014/2015/2016/NC/02	Ukodishaji wa vibanda (Maduka), nafasi 8
LGA/014/2015/2016/NC/03	Ukodishaji wa mabanda ya kuku, nafasi 10
LGA/014/2015/2016/NC/04	Ukodishaji wa maegesho ya magari(magari 20),nafasi 1
LGA/014/2015/2016/NC/05	Ukodishaji wa vyoo, nafasi 1.

**3.MASHARTI YA MWOMBAJI.**

- (I) Muombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri
- (II) Ada ya maombi ya zabuni ni **Tshs. 20,000/=** kwa zabuni, ambazo hazitarudishwa.
- (III) Awe na TIN/VAT kwa anayeomba vibanda. Baada ya kupata kibanda utatakiwa kuwa na leseni ya biashara husika
- (IV) Mzabuni atakaeshinda atatakiwa kuilipa Halmashauri mapato ya mkataba ndani ya siku tano za mwanzo wa kila mwezi.

- (V) Awe mkazi wa kudumu ambaye taarifa zake zipo katika rejesta ya wakazi kwenye vitongoji, kijiji na kata ndani ya halmashauri ya wilaya ya Bagamoyo.
  - (VI) Lazima aonyeshe utambulisho wake wa mkazi (Barua toka Kitongojini, kijijini au Katani)
  - (VII) Awe mfanyabiashara wa mchele na nafaka mbalimbali.
  - (VIII) Awe na uwezo wa kulipa ushuru wa kufanya biashara kwa mkataba wa kwa malipo ya miezi mitatu, miezi sita au mwaka.
  - (IX) Awe na uwezo wa kufanya usafi katika eneo lake la biashara na Kuzipeleka katika eneo la makusanyo ya taka kama watakavyoelekezwa na Halmashauri
  - (X) Kwa waombaji wa vibanda (Maduka) awe tayari kukamilisha ujenzi wa kibanda (Duka) kwa makubaliano na Halmashauri.
4. Vitabu vya Zabuni na maelezo mengine vinapatikana Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, S.L.P. 59, Bagamoyo, (Kitengo cha ununuzi na Ugavi) kuanzia Saa **2.30** asubuhi mpaka **Saa 9.30 alasiri (Jumatatu – Ijumaa)**.
5. Nyaraka za maombi ziwe na nakala **tatu** pamoja na nakala **halisi moja** iliyofungwa kwa **LAKIRI**, iandikwe juu ya bahasha “**NAMBA NA JINA LA ZABUNI ILIYOOMBWA**” na zitumbukizwe katika sanduku la zabuni lililoko Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Zitumwe kwa anwani ifuatayo:

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),  
S.L. P. 59,  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BAGAMOYO.**

6. Mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni tarehe **30/03/2017 saa 4:00 (Nne) asubuhi siku ya** zabuni itafunguliwa muda huo huo katika ukumbi wa mikutano Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya na waombaji mnakaribishwa katika ufunguzi kwa gharama zenu.

*MARY KISIMBO*  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA WILAYA  
BAGAMOYO**